## FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL11

## KISWAHILI PAPER 2 QUESTIONS

# 1. UFAHAMU (Alama 15 )

1. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Tangu opresheni ya Usalama kuanza kutekelezwa na maafisa wa usalama katika mtaa wa Eastleigh, kumekuwa na propaganda kuwa inalenga watu wa jamii na dini Fulani.

Harakati hizi za kuwasaka magaidi sharti ziendelee na zichangiwe na kila raia ili zizae matunda tunayoazimia kupata; kuwanasa wote wanaohusika.

Wakenya tumeishi kwa miaka mingi bila kubaguana katika misingi ya dini na ukabila. Iweje tuanze sasa miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru? Ndiposa tunawasihi Wakenya wote wenye nia njema kukumbuka kwamba hatuna njia ya mkato katika suala hili la ugaidi. Sharti tupambane nao. Hawa ni watu; ni ndugu zetu, rafiki zetu na watoto wetu.

Hakuna mzazi atakayejitokeza hadharani na kukiri kuwa mtoto wake ni gaidi! Hata kama atajua wazi mwanawe ni gaidi na amelipua Wakenya na ataendelea kufanya hivyo akizidi kupewa nafasi. Atanyamaza na kumtetea kwa hali na mali.

Madhara ya mashambulizi hayo ya kigaidi tayari yameanza kuonekana ambapo wamiliki wa mahoteli ya kifahari wanalalama kuwa idadi ya wageni imepungua maradufu. Hali kama hii ni hatari kwa uchumi wa nchi.

Sisi tukiwa Wakenya wapenda amani hatuna budi kuungana mkono katika operesheni hiyo na kushirikiana na maafisa wa usalama kwa kutoa habari muhimu kuhusu washukiwa wa ugaidi. Hakuna operesheni dhidi ya wahalifu ambayo inaweza kuendeshwa bila jamii ambapo wamejificha kuathiriwa.
Heri nusu shari kuliko shari kamili, magaidi wana madhara makubwa kuliko operesheni ya usalama.

Sisi Wakenya kwa sasa tuko katika hali hii tatanishi ya kushindwa kuamua; tupambane na magaidi tuumize Wakenya wachache wasio na hatia ama tuache tu magaidi wakae kwa sababu tunaogopa kuwasumbua hao wachache.

Kadhalika, badala ya kuangazia maeneo yenye visa vingi vya mashambulizi ya ugaidi operesheni ya usalama inafaa kuelezwa pia katika maeneo mengineyo ambayo yamekuwa yakikumbwa na visa vya utovu wa usalama mara kwa mara.

Vikosi vya usalama vinafaa kuhakikisha kuwa magenge ya aina hayasazwi katika operesheni hiyo. Aidha, serikali inapaswa kutoa makataa kwa kila mkenya ambaye anamiliki bunduki kinyume cha sheria kusalimisha silaha hizo mara moja katika vituo vya polisi, la sivyo wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Wakenya wote wafaa kuonyesha ushirikiano kwa kuwa makini zaidi. Wajiepushe na maeneo hatari ambayo yaweza kuwa makazi ya magaidi ama ya washukiwa wa ugaidi. Aliye kando haangukiwi na mti msihausahau msemo maarufu.

**MASWALI**
a) Eleza uongo unaosambazwa kuhusu operesheni ya usalama mtaani Eastleigh. (alama 1)
.......................................................................................................
.......................................................................................................

B)Eleza jinsi Wakenya wamekuwa wakiishi tangu uhuru. (alama 1)
......................................................................................................
......................................................................................................
i) Magaidi wana uhusiano upi kwa mujibu wa kifungu? (alama 1)
......................................................................................................

......................................................................................................
ii) Eleza namna wazazi wanavyochangia kuwepo kwa ugaidi nchini. (alama 2)
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
b) Fafanua athari mbili zinazokumba nchi kutokana na ugaidi. (alama 2)

......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
c) Wakenya wamepewa changamoto ipi ili kusaidia katika kuangamiza ugaidi? (alama 2)
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
d)"Wakenya wako kwenye njia panda". Tetea kauli hii ukirejelea kifungu. (alama 2)
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
e) Serikali inapaswa kuchukua hatua ipi dhidi ya wamiliki haramu wa bunduki. (alama 2)
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................
......................................................................................................

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na kifungu hiki. (alama1)
g) Propaganda
......................................................................................................
......................................................................................................
ii) Makataa (alama1)
......................................................................................................
......................................................................................................

**2. UFUPISHO**

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu; kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kutumikia mwanamume kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga. Mwanamke yeyote ailiyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, aliipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia. Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumnyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa mwaka hadi mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni

yakishangiliwa na kupitishwa,watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa Umoja wa Mataifa wa wanawake (Unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya Umoja wa Mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika Nyanja mbalimbali za maisha; siasa, uchumi, utawala na kadhalika. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu

muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengi. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

a) Bila kubadilisha maana asilia, fupisha aya tatu za kwanza (maneno 45 -55)

**Matayarisho:**

............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................

**Jibu:**

............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................

b) Kwa kurejelea aya mbili za mwisho, eleza maswali muhimu anayoibua mwandishi (maneno 60 -65)

**Matayarisho:**

............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................

**Jibu:**

............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................
............................................................................................

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )

3. a) Eleza maana ya mofimu (alama 2)

..........................................................................................
..........................................................................................

b) Ainisha vivumishi katika sentensi hii: wanafunzi wavulana waliandika insha ngapi za Kiswahili? (alama 3)

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

c) Taja king'ong'o cha kaakaa gumu. (alama 1)

..........................................................................................
..........................................................................................

d) Tunga sentensi moja moja inayodhihirisha matumizi ya maneno yafuatayo: (alama 2)

i) Angalau

..........................................................................................
..........................................................................................

ii) Aghalabu

..........................................................................................
..........................................................................................

e) Kanusha sentensi ifuatayo:

Chakula ambacho kimepikwa sasa kisingalinunuliwa jana kisingaliiva mapema. (alama 3)

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

f) Andika kwa wingi: (alama 2)

Ugomvi ulipozuka pale ulimi wake ulipatapata.

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

g) Yakinisha (alama 1)

Usipojibu swali hii utawaudhi wengi.

..........................................................................................
..........................................................................................

h) Andika kwa udogo (alama 2)

Nguo yake iliraruliwa na mbwa mkorofi.

..........................................................................................
..........................................................................................

i) Tunga sentensi ukitumia neno 'kinanda' kisha ubainishe ngeli yake. (alama 2)

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

j) Andika katika usemi halisi (alama 3)

Afisa alitaka kujua idadi ya mahabusu ambao wangeachiliwa keshoye.

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:

KN( E + N +V) + KT (T) +U+KN (N)+KT (T) (alama 2)

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

m) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendama (alama 2)

Habari za kifo chake zilifichwa

..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

n) Kanusha (alama 2)

Mwanafunzi hodari apongezwa na rais.
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

o) Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kauli mwafaka ya kitenzi ulichopewa. (alama 2)
Kinuthia alipo………………….. (fa) mwanawe kwa kumpiga, haku… ....... (wa) radhi na mahakama

p) Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi ifuatayo:
Twendeni tuone mhubiri ni nani? (alama 3)
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

q) Tambua chagizo (alama 2)
Ninaenda Nakuru lakini nitarudi saa moja
..........................................................................................

r) Unda nomino mbili kutokana na neno hudumu (alama 2)
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

s) Kanusha sentensi hii kwa kutumia kiwakilisho amba (alama 2)
Ubao upakwao rangi hupendeza
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

t) Ala tuli ni nini? (alama 1)
..........................................................................................
..........................................................................................

## 4. ISIMU JAMII (Alama 10 )

4. a) Usanifishaji wa lugha ni nini? (alama 2)
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

b) Ni nini umuhimu wa kusanifisha lugha ya Kiswahili? (alama 8)
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................